

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.LDC/L.10/13 VOL.V/04

Tarehe. 17/09/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA KWA KUSHIRIKIANA NA SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA ANATANGAZA NAFASI ZA KAZI ZA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III KAMA IFUATAVYO:-

MTENDAJI WA KIJIKI III – NGAZI YA MSHAHARA TGS B (NAFASI 8)

1. SIFA ZA KUAJIRIWA

Kuajiriwa mwenye elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo; Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na serikali.

2. KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI III

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- ii. Kusimamia Ulinzi na usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- iv. Katibu wa mikutano na kamati zote zote za halmashauri ya kijiji
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- vi. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za kijiji.
- vii. Kujibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha Wananchi kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa Njaa, Umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- viii. Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya Wananchi
- ix. Kusimamia utungaji na utekelezaji wa Sheria ndogo za Kijiji
- x. Kuibua vyanzo vya mapato na kusimamia ukusanyaji wa Mapato katika Kijiji
- xi. Kuandaa na kutunza Rejesta za Wakazi wote katika Kijiji

3. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE.

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji wote wawe na umri wa miaka 18 hadi 45.
- iii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iv. Waombaji wote wanatakiwa kuwa na Namba ya Utambulisho wa Uraia (National Identification number) kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- v. **Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.**
- vi. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimekaguliwa na kuthibitishwa na na mamlaka husika (NECTA, NACTE na TCU)
- viii. Waombaji wote kwenye barua zao za maombi waandike namba za simu za uhakika kwa ajili ya mawasiliano.
- ix. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa ya kazi husika. Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.
 - Diploma/Certificates.
 - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
 - Picha mbili "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- x. **"Transcripts", "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV and FORM VI results slips) Havitakubaliwa.**
- xi. **Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.**
- xii. **Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 01/10/2021 saa 09:30 Alasiri.**

4. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Maombi yatumwe yakiwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia anuani ifuatayo:-

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA,
S.L.P 19,
LUDEWA.**

Tangazo hili limetolewa na:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
LUDEWA.